

HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)

Simu Mkurugenzi: 255-28-2501375

Ofisi zote: 255-28-2540334

Fax: 255-028-2500785

Email: mwacity@thenet.co.tz



S.L.P. 1333,
MWANZA.

Kumb. Na. MCC/S.10/5/88

08 Mei, 2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

AGPAHI ikishirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza inakusudia kuajiri wataalam wa kada za afya katika kituo cha **Afya cha Igoma** kilichopo katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza kama ifuatavyo;

1. TABIBU II (CLINICAL OFFICER II) – NAFASI 2

a. Sifa za kuajiriwa

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye Stashahada ya Tabibu/Tabibu Meno kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

b. Kazi na majukumu:

- i. Kazi zote zinazofanywa na Tabibu Msaidizi
- ii. Kutambua na kutibu magonjwa ya kawaida
- iii. Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake na kufanya upasuaji mdogo
- iv. Kushiriki katika kupanga na kutekeleza Huduma za Afya Msingi
- v. Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za Afya za Mfuko wa Afya ya Jamii
- vi. Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma
- vii. Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji
- viii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

c) Ngazi ya Mshahara

Kiwango cha Mishahara ya Serikali TGHS B.

2. MTEKNOLOJIA (MAABARA) II (TECHNOLOGIST (LAB) II) - NAFASI 5

a) Sifa za kuajiriwa

Kuajiriwa wenye Stashahada (Diploma) katika fani ya Uteknolojia wa Maabara, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa .

b) Kazi na Majukumu:

- i. Kupima sampuli zinazoletwa maabara.
- ii. Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa Maabara za ngazi za juu.
- iii. Kufanya kazi za ukaguzi wa maabara, vitendanishi, vifaa, kemikali na hifadhi ya kemikali
- iv. Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi.
- v. Kufundisha watumishi walio chini yake.
- vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

c) Ngazi ya Mshahara

Kiwango cha Mishahara ya Serikali TGHS B.

3. SIFA ZA WAOMBAJI KWA UJUMLA

Mwombaji wa nafasi ya kazi anatakiwa;

- i. Awe raia wa Tanzania
- ii. Awe na umri kati ya miaka 20 – 40
- iii. Awe hajawahi kushitakiwa na kufiwa hatiani kwa makosa ya jinai

4. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

Maombi yaandikwe kwa mkono na kuambatishwa na nakala za vyeti vya elimu na taaluma pamoja na maelezo binafsi (CV) ambayo imechapwa na kusainiwa mwombaji kasha yatumwe kwa anwani ifuatayo;

Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya Jiji la Mwanza,
S.L.P. 1333,
MWANZA.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15 Mei, 2018 saa 08.30 alasiri.